



Australian Government



# Kutarajia nini siku ya chanjo ya COVID-19 katika kituo chako cha huduma cha wazee wa makazi

## Habari kwa wakazi, familia, watunzaji na wapendwa

Serikali ya Australia ina mkakati wa kutoa chanjo za COVID-19 kwa kila mtu anayeishi Australia.

Wafanyakazi na wakazi wa huduma za wazee wa makazi watakuwa miongoni mwa watu wa kwanza ambao wanaweza kuchagua kupokea chanjo ya COVID-19. Hii ni sehemu ya [awamu ya kwanza \(Awamu ya 1a\) ya mkakati wa kitaifa cha kutolewa chanjo ya COVID-19](#).

Chanjo ya COVID-19 kwa wafanyakazi na wakazi wa huduma ya wazee wa makazi itafanyika katika vituo vya huduma za wazee wa makazi. Kituo chako cha huduma za wazee wa makazi kitakujulisha wakati itakuwepo siku yako ya chanjo.

Hati hii inakupua wewe, familia yako, watunzaji na wapendwa habari kuhusu nini unachoweza kutarajia katika kipindi kabla, na siku yako ya chanjo.

## Kabla ya siku ya chanjo

- Serikali ya Australia itasimamia kwa chanjo kutolewa kwenye kituo chako cha huduma ya wazee wa makazi.
- Serikali ya Australia pia imepata wafanyakazi wa afya ambao watatembelea kituo chako cha huduma za wazee wa makazi na kusimamia chanjo kwa wakazi na wafanyakazi. Wafanyakazi hawa wa afya watashirikiana kwa karibu sana na kituo chako katika kipindi kabla siku ya chanjo ili kupanga na kuhakikisha siku ya chanjo inaenda salama na kwa ufanisi.
- Kituo chako cha huduma cha wazee wa makazi kitaomba wewe, na mwamuzi mbadala wako (ikiwa mmoja yuko), kukubali kupokea chanjo ya COVID-19.
  - Maelezo yanapatikana kwako ili uweze kuamua uamuzi sahihi kuhusu chanjo ya COVID-19. Ikiwa hujawahi kutolewa na habari hii na kituo chako, unaweza kupata nakala kwenye [tovuti ya Idara ya Afya](#).
  - Kabla ya kutoa idhini, wewe, familia yako, watunzaji na watoa maamuzi unaweza pia kuchagua kujihusisha na wafanyakazi wa afya katika kituo chako, GP au wataalamu wengine wa afya kujadili faida na hatari za chanjo, na kama ni mzuri kwa wewe kupata chanjo ya COVID-19.
- Wafanyakazi wa afya katika kituo chako wataangalia afya yako ili kuhakikisha kuwa inafaa kwako kupokea chanjo. Ikiwa kituo chako kina wasiwasi wowote kuhusu afya yako watashauriana na GP. Unaweza pia kuchagua kuzungumza na GP yako wakati wowote kuhusu afya yako na chanjo ya COVID-19.
- Ikiwa unakubali kupokea chanjo ya COVID-19 kituo chako cha huduma za wazee wa makazi kitakusajili kupokea chanjo. Kituo chako kitasimamisha mipango yote kwa siku ya chanjo na wafanyakazi wa chanjo.
- Chanjo ya COVID haina haja ya kuagizwa kwako na GP yako.
- Una haki ya kupata mtetezi wa huduma ya wazee. Huduma hii kupitia OPAN ni bure, siri na huru ya serikali na watoa huduma wa wazee. Watetezi wa Huduma ya Wazee katika jimbo au wilaya yako wanapatikana kwenye 1800 700 600 au kwenye [opan.com.au](#).

## Siku ya chanjo

- Ikiwa unakusudia kupokea chanjo, wafanyakazi wa afya katika kituo chako wataangalia kuhakikisha uko mzima siku ya chanjo. Ikiwa unapata shida ya afya kwa siku ya chanjo kituo chako cha huduma ya wazee wa makazi kinaweza kushauriana na GP ili kuamua kama chanjo yako inaweza kupewa, au ikiwa inahitaji kuchelewa hadi tarehe ya baadaye.
- Unaweza kuchagua kuwa na mtu wa msaada kuja kituo chako cha huduma ya wazee wa makazi kwa siku ya chanjo ili kukusaidia na kuunga mikono. Hii inaweza kujumuisha mtu kutafsiri habari au kutoa uhakika ikiwa unajisikia wasiwasi.
- Kama ilivyo na chanjo yoyote, unaweza kuwa na madhara fulani baada ya kupokea chanjo ya COVID-19. Taarifa kuhusu kutarajia nini baada ya chanjo yako itapewa kwako na mfanyakazi wa afya anayetoa chanjo yako. Habari hii inapatikana pia kwenye [tovuti ya Idara ya Afya](#).
- Baada ya chanjo yako, wafanyakazi katika kituo chako cha huduma za wazee wa makazi watafuatilia kwako karibu. Ikiwa unajisikia mgonjwa baada ya kupokea chanjo yako hakikisha uwaambie hivyo.

## Endelea kusasisha na maelezo ya kuaminika

Unaweza kupata maelezo zaidi, ikiwa ni pamoja na maelezo ya kutafsiriwa juu ya Idara ya Afya [Tovuti ya chanjo za COVID-19](#). Unaweza pia kujiunga ili kupokea [sasisho za chanjo za COVID-19](#).

Unaweza pia kupiga simu kwa Simu ya Msaada ya Kitaifa ya Virusi vya Korona kwenye 1800 020 080, na kuomba mkalimani kama inahitajika.

[Mtandao wa Utetezi wa Watu Wazee \(OPAN\)](#) unapatikana ikiwa unataka kuzungumza juu ya masuala yoyote au wasiwasi unayo kuhusiana na COVID-19 au kama unahitaji msaada kujihusisha na mtoa huduma yako ya wazee. Piga simu kwa 1800 237 981, saa 12 asubuhi hadi saa 4 usiku (6am-10pm) (AEDT), siku 7 ya wiki au tuma barua pepe kwa [covid@opan.com.au](mailto:covid@opan.com.au).